



## Kuunganishwa na kila mmoja

Waunganishaji wanafanya kazi na watu wote na jamii, ikiwa ni pamoja na watu kutoka tamaduni na asili tofauti, na jamii za asili au Aborijino. Waunganishaji watakusaidia kuweza kuwa sehemu ya jamii ya mahali na iliyopanuliwa.

Unaweza kuwasiliana na Muunganishaji wakati wowote unapohitaji, na katika njia inayokufaa.

Kazi ya muunganishaji ni kuweza kutoa msaada wa mda mfupi ili kuweza kufikia malengo fulani.

Mtu anaweza kuwasiliana na waunganishaji tena siku zijazo kama hitaji lingine limejitokeza au msaada zaidi au habari zinatakiwa.



*Linking people and communities with opportunities*

Kuwasiliana katika Kiswahili, tafadhali pigia Huduma ya Ukalimani na Utafsiri wa Lugha (TIS) kwa 131 450.

# ABILITY LINKS

NEW SOUTH WALES

## Kuunganisha watu kwenye jamii ya mahali



*Linking people and communities with opportunities*

# Waunganishaji wanaweza kukusaidia

Kutafuta njia  
ya kuwa sehemu  
ya jamii

Kujenga  
kujiamini ili kufikia  
malengo yako

Kukuza marafiki  
waliopo mnaosaidiana nao  
na kujenga marafiki wapya

Kupanga mipango  
na matarajio ya  
siku zijazo

## Nini maana ya Ability Links NSW?

Ability Links NSW inasaidia watu wenye ulemavu, familia zao na walezi kuweza kuishi maisha wanayoyataka, kama wana jamii wanaothaminiwa kwenye jamii yao.

Inafanya hivi kwa kuunganisha watu kwenye jamii zao.

Kwa kupitia waunganishaji wa mahali husika, Ability Links NSW inasaidia pia jamii kuweza kuhusika ipasavyo.

Ability Links NSW ni Mpango wa Idara ya Serikali ya NSW ya Familia na Huduma za Jamii, Uzee, Ulemavu na Matunzo ya Nyumbani

## Ni namna gani Ability Links NSW inafanya kazi?

Waratibu wa Ability Links NSW, wanaojulikana kama Waunganishaji (Linkers), wanafanya kazi kwa karibu na watu wenye ulemavu, familia zao na walezi ili kuwasaidia kuweza kutimiza malengo yao, matumaini na ndoto.

Kama lengo ni kushiriki katika michezo, elimu, kujitolea, au shughuli nyingine, wewe unabakia unabaki na sehemu kubwa katika kufanya maamuzi kuhusu jinsi gani unataka kuishi maisha yako.

Waunganishaji wana uelewa wa mahali na wanafanya kazi pamoja na jamii, kuzisaidia ili ziwe za kukaribisha na kujumuisha.



## Nani anaweza kusaidiwa na Ability Links NSW?

Ability Links NSW ni kwa ajiri ya:

- watu wenye ulemavu kuanzia miaka 9 mpaka 64
- walezi na familia wa watu wenye ulemavu.

Watu binafsi, virabu, makundi na wafanya biashara wanaweza kusaidiwa pia na Ability Links NSW kwa habari na msaada wa jinsi ya kuwashirikisha watu wenye ulemavu.

Hakuna tathmini ya kisheria inayotakiwa ili uweze kupata msaada au kuunganishwa nasi ili uweze kusaidiwa na Ability Links NSW.